



Shalom,Jina la Mwokozi wetu Yesu Kristo lihimidiwe milele....

Karibu tujifunze Maneno ya Uzima kwa njia ya ndoto....Kama una ndoto inakutatiza basi usisite kuiandika kwenye box la maoni chini....

Ndoto ya kuota umekufa uwa ina maana nyingi kulingana na ujumbe ambaulipaswa kufika mahali husika...

Ikiwa umeota ndoto hii na unaona ndani yako una msukumo wa kufahamu maana yake basi ujue kuna jambo Mungu anataka ulifahamu

Ikiwa wewe ni Mke au mume wa mwingine na umekuwa na tabia ya kufanya mambo ya uzinzi na usharati kwa siri basi fahamu kabisa kifo kipo katikati yako..Kwsababu Biblia inasema katika wanandoa kifo ndio kitakachowatenganisha...

Mwanzo 20:3

[3]Lakini Mungu akamjia Abimeleki katika ndoto ya usiku, akamwambia, Umekuwa mfu wewe kwa sababu ya mwanamke huyu uliyemtwa, maana ni mkewe mtu.

Kwa kulifahamu hilo yakupasa haraka sana uache mwenendo wako huo mbaya na utubu dhambi zako na uishi maisha Matakatifu...

Ikiwa tabia yako sio hiyo ya kwanza

Basi fahamu kuwa ni maisha yako ya Kiroho yapo chini sana,huenda umekuwa mtu wa kupenda anasa sana,Mambo ya ulimwengu huu, usiyeweza kujizuia...Hivyo ikiwa ni mtendaji wa mambo hayo hapo unajulishwa umekuwa mfu...

Na suluhisho ni Kumwamini Yesu Kristo na kutubu dhambi zako zote kwa kumaanisha



kuziacha na kubatizwa ubatizo sahihi wa maji Mengi na kwa jina lake Yesu Kristo..

1 Timotheo 5:6

[6]Bali, yeye asiyejizuia nafsi yake amekufa ingawa yu hai.

Shalom.....